

Je! sisi ni wafalme na makuhani kwa namna gani?

SWALI: Yohana hapa anasema Bwana ametufanya kuwa Ufalme na Makuhani Ufunuo 1:6 ... (Sasa hapa anamaanisha sasa hivi sisi ni wafalme na makuhani au ni katika ule umilele ujao?) na je! ni sahihi kumuita mwanamke kuhani??

JIBU: Ndio sasahivi sisi ni ufalme na makuhani wa Bwana katika roho...kama vile Bwana Yesu alivyokuwa duniani tangu siku za kuzaliwa kwake mpaka siku za kuondoka kwake,...tayari yeye alishakuwa mfalme...Kama unakumbuka wale Mamajusi walimuuliza Herode yuko wapi mfalme wa wayahudi tunataka kumsujudia (Mathayo 2:3)? unaona hapo tangu alipokuwa mdogo tayari ni mfalme, pia Pilato tunaona baadaye siku chache kabla ya kuondoka kwake duniani alikuja kumuuliza Bwana ...

Yohana 18: 33 "Basi Pilato akaingia tena ndani ya Praitorio, akamwita Yesu, akamwambia, Je! Wewe ni Mfalme wa Wayahudi?

34 Yesu akajibu, Wewe wasema hivi kwa nafsi yako, au watu wengine walikuambia habari zangu?

35 Pilato akajibu, Ama! Ni Myahudi mimi! Taifa lako na wakuu wa makuhani ndio waliokuleta kwangu. Umefanya nini?

36 Yesu akajibu, Ufalme wangu sio wa ulimwengu huu. Kama ufalme wangu ungekuwa wa ulimwengu huu, watumishi wangu wangenipigania, nisije nikatiwa mikononi mwa Wayahudi. Lakini ufalme wangu sio wa hapa.

37 Basi Pilato akamwambia, Wewe u mfalme basi? Yesu akajibu, Wewe wasema, kwa kuwa mimi ni mfalme. Mimi nimezaliwa kwa ajili ya haya, na kwa ajili ya haya mimi nalikuja ulimwenguni, ili niishuhudie kweli. Kila aliye wa hiyo kweli hunisikia sauti yangu".

Kwahiyo hata sisi tuliookolewa, na kuoshwa kwa damu ya Bwana wetu Yesu Kristo, ni makuhani na ufalme. Lakini mambo hayo yatakuja kudhihirika katika ulimwengu unaokuja kama Bwana alivyosema ufalme

Je! sisi ni wafalme na makuhani kwa namna gani?

wake ni wa ulimwengu unaokuja!...Na ukuhani wenyewe hautakuwa wa kuvukiza uvumba tena, ule ulikuwa ni taswira ya mambo yatakayokuja yanayofunua kumkaribia Mungu..

Vivyo hivyo na katika huo ulimwengu unaokuja hatutakuwa tu wafalme bali tutakuwa na uwezo kumkaribia Mungu kwa namna ya kipekee mfano wa makuhani, ambao sio watu wote watapewa uwezo huo bali ni wale watakaoshinda tu!.. Na thawabu hiyo itakuwa ni kwa wote...wanawake na wanaume.

Hivyo ukuhani wako mbele za Mungu unautengeneza ukiwa hapa hapa duniani, kwahiyoo tunapaswa tukaze mwendo ili tusikose thawabu hiso.

Ubarikiwe sana.

Mada zinazoendana:

TUMEFANYIKA KUWA WANA WA MUNGU!

MAVAZI YA NDANI NA YA NJE.

Je! sisi ni wafalme na makuhani kwa namna gani?

TUZO UTAPEWA KULINGANA NA NAFASI YAKO.

UNALITUMIA KWA HALALI NENO LA KWELI?

NI NANI ALIYEIDHARAU SIKU YA MAMBO MADOGO?

UTENDAJI KAZI WA MPINGA-KRISTO.

Rudi Nyumbani:

Share on:

WhatsApp